

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA



KONGAMANO LA BIASHARA NA UWEKEZAJI KATI YA TANZANIA NA JAMHURI YA CZECH LITAKALOFANYIKA KWENYE MJI WA PRAGUE, TAREHE 2 MEI, 2017.

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Taasisi ya Sekta Binafsi ya Tanzania (TPSF); Ofisi ya Balozhi wa Heshima wa Jamhuri ya Czech nchini Tanzania kinaratibu Kongamano la Biashara na Uwekezaji Kati ya Tanzania na Jamhuri ya Czech litakalofanyika tarehe 2 Mei, 2017 katika mji mkuu wa Czech, Praque. Lengo la kongamano hili ni kuwakutanisha ana kwa ana wafanyabiashara/wawekezaji wa nchi hizi mbili ili kujadiliana fursa mbalimbali za kibiashara na uwekezaji zitakazowezesha kuanzisha na kuendeleza miradi ya viwanda, kupata wabia wa kuleta mitaji ya biashara, teknolojia pamoja na kupata masoko.

Sekta zilizolengwa ni kilimo (korosho, viungo, kahawa, chai, mahindi, pamba, katani, alizeti, ufuta): Teknolojia; mawasiliano; utalii, madini na biashara kwa ujumla.

Tunategemea Tanzania itaongeza thamani ya mitaji ya uwekezaji kutoka nje (FDI) iwapo makampuni ya wafanyabiashara kutoka Jamhuri ya Czech na Tanzania yatakubaliana kufanya biashara na kuwekeza Tanzania. TIC inapenda kutumia fursa hii kuwatangazia wafanyabiashara nchini kushiriki kongamano hili.

Wafanyabiashara watakaopenda kushiriki kongamano hili watahitajika kujiandikisha TIC kabla ya tarehe 25 April, 2017 kwa (Bi. Latiffa Kigoda kwa simu na. 0715734444 /latiffa.kigoda@tic.co.tz) au (Bw. Ayoub Magarya kwa simu na. 0654862931/ ayoub.magarya@tic.co.tz). Programu ya kongamano itatumwa kwa washiriki mara baada ya kuthibitisha ushiriki wao.